الطهارة والصلاة - سواحيلي

# TWAHARA NA SWALA



جمعية الدعوة بالزلفي


جمعية الدعوة والإرشاد وتوعية الجاليات بالزلفي

هاتف:٤٢٣٤٤٦٦ ٠١٦ ـ فاكس:٤٢٣٤٤٧٧ ٠١٦

# TWAHARA NA SWALA

## الطهارة والصلاة - سواحيلي


جمعية الدعوة والإرشاد وتوعية الجاليات في الزلفي

هاتف: 966 164234466 ـ فاكس: 966 164234477

# الطهارة والصلاة - سواحيلي

**أعده وترجمه للغة السواحيلية**

**جمعية الدعوة والإرشاد وتوعية الجاليات بالزلفي**

**الطبعة الأولى: ١٤٤٤/٠٦ هـ**


**ⓒ جمعية الدعوة والإرشاد وتوعية الجاليات بالزلفي ، ١٤٤٤هـ**

***فهرسة مكتبة الملك فهد الوطنية أثناء النشر***

جمعية الدعوة والإرشاد وتوعية الجاليات بالزلفي
الطهارة والصلاة / لغة السواحلية. / جمعية الدعوة والإرشاد
وتوعية الجاليات بالزلفي .- الزلفي ، ١٤٤٤هـ
٤٨ ص ؛ ..سم

ردمك: ٤-٠٦-٨٣٩٩-٦٠٣-٩٧٨

١- الطهارة ( فقه اسلامي ) 2- الصلاة أ.العنوان
ديوي ٢٥٢ ١٤٤٤/٥٨١٧

**رقم الإيداع: ١٤٤٤/٥٨١٧**
**ردمك: ٤-٠٦-٨٣٩٩-٦٠٣-٩٧٨**

# HUKMU ZA TWAHARA

# أحكام الطهارة

## TWAHARA NA NAJISI.

**NAJISI YA HISIYA**, ni najisi ambayo ni wajibu juu ya muislamu kuisafisha na kuiondoa na kuosha sehemu iliyopatwa na najisi hiyo.

Ni wajibu kuosha nguo na mwili viliyoingiwa na najisi hiyo mpaka iondoke sehemu iliyoingia, ikiwa najisi inaonekana kama vile damu ya hedhi itaoshwa, ikiwa itabakia athari yake kutokana na ugumu wa kutoka basi itaachwa hakuna tatizo kwa kubaki kwa athari yake.

Ikiwa najisi haionekani inatosha kuosha sehemu hiyo hata kama ni mara moja inatosha.
Ikiwa najisi imesambaa ardhini kutwaharishwa kwake ni kumwaga maji juu yake, kama ambavyo kutwaharishwa kwake ni kukauka kwa najisi ikiwa ni ya umajimaji.

Ama ikiwa najisi ni ya athari sio maji maji haitwaharishwi kwa maji isipokuwa itaondolewa na kwenda kutupwa kama vile kinyesi cha mbwa n.k.

Hutumika maji katika kutwaharisha na kuondoa najisi, kama vile maji ya mvua, maji ya bahari, maji ya mto na maji mengineyo ambayo ni twahara.

Kama ambavyo inafaa kuyatumia maji yaliyotumika ambayo hayaja badilika, na vile vile inafaa kuyatumia maji ambayo yamechanganyika na kitu ambacho ni twahara, maji yatabaki katika asili yake hayatabadilika.

Lakini maji yakichanganyika na kitu ambacho ni twahara, lakini yakabadilika maji hayo kutoka kwenye asili yake ya maji hayatafaa kujitwaharishia, kama vile soda, chai n.k.

Vile vile haifai kuyatumia maji yaliyo changanyika na najisi, ikawa najisi imeyabadilisha maji ladha yake, harufu yake na rangi yake.

Ikiwa najisi haijayabadilisha maji chochote katika hizo sifa tulizo zitaja hapo, basi maji hayo hayatafaa kuyatumia katika kauli sahihi ya wana wavyuoni.

Vile vile inafaa kuyatumia maji yaliyobaki kwenye chombo baada ya kunywewa, isipokuwa ikiwa ameyanywa mbwa au nguruwe maji hayo yatakuwa ni najisi hayatafaa kujitwaharishia.

## AINA ZA NAJISI.

Najisi inayotoka katika njia mbili tupu ya mbele na tupu ya nyuma zipo aina nyingi miongoni mwazo ni;

1. Mkojo na haja kubwa.
2. Wadiyi ni umaji maji mweupe mzito unaotoka baada ya mkojo.
3. Madhiyi ni umaji maji unaoshikana unatoka wakati wa hisia.
4. Ama manii ni twahara, lakini inapendezwa yaoshwe yakiwa bado hayajakauka, na yapikichwe au kusuguliwa yakiwa yamekauka.
5. Mikojo au kinyesi cha mnyama ambaye nyama yake hailiwi ni najisi, lakini mkojo au kinyesi cha mnyama ambaye nyama yake inaliwa sio najisi.
6. Damu ya hedhi na damu ya nifasi (kujifungua) ni najisi.

Najisi zote hizo tulizozitaja hapo juu ni lazima zisafishwe kwa kutumia maji, na kuziondoa sehemu zilizopo kwenye nguo au mwili isipokuwa manii ya binadamu.

Ama madhiyi ikiwa yataingia kwenye nguo inatoka kwa kuyasafisha kwa kuyarashia maji tu.

## MIONGONI WA HUKUMU ZA NAJISI.

1. Mtu akipatwa na kitu akawa haelewi je, ni najisi au sio najisi? Sio lazima yeye kujiuliza swali hilo, itamuwajibikia yeye kuiosha hiyo sehemu, kwani asili ya kila kitu ni **TWAHARA**.
2. Ikiwa mtu amemaliza kusali akaangalia mwilini kwake au kwenye nguo yake kuna najisi hakuwa ni mwenye kujua tokea mwanzo, au alikuwa anajua lakini akasahau, swala yake itakuwa sahihi katika kauli sahihi ya wanavyuoni.
3. Ikiwa sehemu yenye najisi haionekani kwenye nguo na mfano wake, ni wajibu juu yake kuiosha sehemu anayodhania kuwa najisi imekuwa hapo, kwani najisi inayoonekana ina rangi yake, ladha yake au harufu yake, ikiwa dhana yake haelewi sehemu iliyopo najisi basi ataiosha nguo yote.

## KUKIDHI HAJA

Miongoni mwa adabu za kukidhi haja ni kama ifuatavyo;
1. Kutanguliza mguu wa kushoto na atasema kabla ya kuingia chooni: {Bimsillah ewe mwenyezi mungu najikinga kwako kutokana na mashetani waovu wa kiume na mashetani waovu wa kike} (Allahumma Inni Au'udhubika minal Khubuthi Wal khabaaithi) na

atasema baada kutoka: (Nakuomba msamaha wako) (Ghufraanaka) akitanguliza mguu wake wa kulia.

يقول قبل دخول الخلاء: (بسم الله، اللهم إني أعوذ بك من الـخُـبْث والخبائث)، ويقول بعد الخروج: (غفرانك) مقدمًا رجله اليمنى.

Asiwe amebeba kitu ambacho ndani yake kuna utajo wa Allah, isipokuwa atakapoechelea kitu hicho kupotea kupotea.

2. Asielekee kibla wala kukipa mgongo kibla wakati wa kukidhi haja kwenye sehemu ya wazi, ama sehemu ya nyumba inafaa kukipa mgongo kibla bila ya kukielekea.

3. Kujisitiri tupu kutoka kwenye macho ya watu na kutobweteka kwenye hilo, na tupu ya mwanamume ni kuanzia kitovuni mpaka magotini na tupu ya mwanamke ni mwili wake wote.

4. Kujihifadhi na kujiepusha mwili wake au nguo zake kupatwa na mkojo au kinyesi.

5. Kujisafisha na maji baada ya kukidhi haja au kutumia tishu au mawe na mfano wake kwa ajili ya kuondoa athari ya najisi kwa kutumia mkono wake wa kushoto katika kujisafisha.

# UDHU.

Haikubaliwi swala ya mtu bila ya kuwa na udhu. Hadithi iliyopokelewa na Abi Huraira (R.A) Mtume (saw) anasema ("Hakika ya Mwenyezi Mungu haikubali swala ya mmoja wenu pindi anapotokwa na udhu mpaka atawadhe") (Ameipokea Bukhar na Muslim:6954, 225).

فعن أبي هريرة - ﵁ - أن رسول الله - ﷺ - قال: ((إن الله لا يَقبلُ صلاة أحدكم إذا أحدث حتى يتوضأ)) [متفق عليه:٦٩٥٤، ٢٢٥]

Hapana budi anapo tawadha afuate taratibu na kufuatiliza kiungo kimoja baada ya kingine wakati wa kutawadha.

Udhu una fadhila kubwa sana inatakikana mtu apate hisia ya kuwa anafanya kitu chenye thamani kubwa, kama ilivyo kuja kwenye hadithi ya Swahaba mkubwa wa Mtume (saw) Othman bin Affaan (R.A) anasema, amesema bwana Mtume (saw): (Mwenye kutawadha akaufanya uzuri udhu wake, yatatoka madhambi yake kutoka mwilini mpaka chini ya kucha zake) (Ameipokea Imamu Muslim: 245).

عن عثمان بن عفان - ﵁ - قال: قال رسول الله ﷺ: ((من توضأ فأحسن الوضوء، خرجت خطاياه من جسده، حتى تخرج من

تحت أظفاره )) [رواه مسلم: ٢٤٥ ]. وعنه ـ رضي الله عنه ـ قال: قال رسول الله ﷺ:
(( من أتمَّ الوضوءَ كما أمرَ اللهُ تعالى، فالصلوات المكتوبات
كفارات لما بينهن )) [رواه مسلم: ٢٣١ ].

Na imepokelewa kutoka kwa Othman (R.A) ya kuwa Mtume (saw) anasema:( Mwenye kutimiza udhu kama alivyo amrishwa na Mwenyezi Mungu, basi swala tano za faradhi ni kafara la kufutiwa madhambi kati ya kila swala) (Ameipokea Imam Muslim:231).

## NAMNA YA KUTAWADHA.

1. Atanuia kutawadha moyoni mwake bila ya kutamka kwa ulimi, na nia ni kuazimia jambo au kitu moyoni, kisha atasema Bismillah.
2. Kisha ataosha viganja vyake mara tatu.
3. Kisha atasukutuwa na kupandisha maji puani mara tatu.
4. Kisha ataosha uso wake mara tatu, kuanzia sikio mpaka sikio upana, na kuanzia sehemu iliyoota nywele kichwani mpaka chini ya kidevu urefu.
5. Kisha ataosha mikono yake mara tatu, kuanzia kwenye vidole mpaka kwenye kongo mbili, kwa kuanzia mkono wa kulia kisha mkono wa kushoto.
6. Kisha atapangusa kichwa chake mara moja, ailoweshe mikono kisha aipitishe kuanzia mwanzo wa

kichwa mpaka nyuma ya kichwa kisha airudishe mpaka mwanzo alipoanzia.

7. Kisha apanguse masikio yake mawili, aingize vidole vyake vya shahada kwenye tundu za masikio, na utapangusa juu ya masikio yake mawili kwa vidole gumba.

8. Kisha ataosha miguu yake miwili mara tatu, kuanzia kwenye vidole pamoja na nguyu mbili (vifupa viwili vilivyoko mguuni) akianzia mguu wa kulia kisha mguu wa kushoto.

9. Kisha inapendeza akiwa ataomba dua hii iliyokuja baada ya kumaliza kutawadha:

أشهد أن لا إله إلا الله، وأنَّ محمدًا عبده ورسوله

(Nashudia ya kwamba hapana mola anaestahiki kuabudiwa kwa haki isipokuwa Mwenyezi Mungu pekee, na ninashudia ya kwamba hakika ya Muhammad ni mja wake na Mtume wake.)

فعن عمر بن الخطاب ـ رضي الله عنه ـ قال: قال رسول الله ﷺ: ((ما مِنكُم من أحد يتوضأ فيسبغ الوضوء ثم يقول: أشهد أن لا إله إلا الله، وأنَّ محمدًا عبده ورسوله، إلاَّ فُتحت له أبواب الجنة الثمانية، يدخل من أيها شاء )) [ رواه مسلم: ٢٣٤ ].

Hadithi aliyoipokea swahaba Umar bin Khatwab (R.A) anasema: Amesema bwana Mtume (saw) kuwa:

(Hayupo yeyote miongoni mwenu akatawadha akaufanya vizuri udhu wake kisha akasema: Nashuhudia ya kuwa hapana mola apasae kuabudiwa kwa haki isipokuwa Mwenyezi Mungu, na ninashudia ya kuwa Muhammad ni mja wake na Mtume wake, isipokuwa atafunguliwa siku ya kiyama milango minane ya peponi, aingie mlango wowote autakao) (Ameipokea Imamu Muslim: 234).



## KUPANGUSA KHOFU MBILI.

Kutokana na uzuri na wepesi wa dini ya kiislamu ni kuruhusu au kujuzisha kupangusa juu ya khofu mbili, nayo imethibiti kwa bwana Mtume (saw) kwa hadithi aliyoipokea Swahaba Amru bin Umaiyya (R.A) anasema:

فعن عمرو بن أُمية - رَضِيَ اللَّهُ عَنْهُ - قال: (رأيتُ النبي - صَلَّى اللَّهُ عَلَيْهِ وَسَلَّمَ - يَمسحُ على عِمَامته وخُفَّيه) [رواه البخاري: ٢٠٥]

(Nilimuona Mtume (saw) akipangusa juu ya kilemba chake na juu ya khofu zake mbili) (Ameipokea Imamu Bukhar: 205).

وعن المغيرة بن شعبة - رَضِيَ اللَّهُ عَنْهُ - قال: (بينا أنا مع رسول الله - صَلَّى اللَّهُ عَلَيْهِ وَسَلَّمَ - ذات ليلة، إذ نَزَل فقضى حاجته، ثم جاء فصببت عليه من إداوةٍ كانت معي فتوضأ ومسح على خفيه) [متفق عليه:٢٠٣،٢٧٤]

Ameipokea Swahaba Mughira bin Shu'ubah (R.A) anasema:( Wakati tukiwa mimi pamoja na Mtume wa Mwenyezi Mungu siku moja, muda kidogo akaenda kukidhi haja yake, kisha akaja nikammiminia maji yaliyoko kwenye chombo nilichokuwa nacho akatawadha na akapangusa juu ya khofu zake) (Ameipokea Bukhar na Muslim:203, 274).

Ni sharti kwa mwenye kupangusa juu khofu zake azivae akiwa ametawadha tayari, na iwe kupangusa ni kupitisha mikono iliyolowa maji apanguse juu yake, wala asipanguse chini ya khofu.

Muda wa kupangusa kwa mkazi wa mji ni siku moja mchana na usiku yaani masaa 24 tu, na muda wa kupangusa kwa msafiri ni siku tatu na masiku yake, lakini ni yule msafiri ambae safari yake ni ile ambayo anafaa kunguza swala.
Na inabatilika kupangusa juu ya khofu kwa kuisha muda wake au mtu akazivua baada ya kupangusa, au baada ya kupatwa na janaba hapo itamlazimu kuzivua ili aweze kuoga.

## VYENYE KUTENGUA UDHU.

1. Chenye kutoka moja ya njia mbili (njia ya mbele au nyuma) mkojo, haja kubwa, kujamba, manii, madhiyi, wadiyi, damu nyingi,
2. Kulala,
3. Kula nyama ya ngamia,
4. Kuzimia na kupotewa na akili.

## KUOGA (JOSHO)

Kuoga ni kueneza maji mwili mzima kwa nia ya kujitwaharisha, ni lazima katika kuoga ni kuuosha

mwili wote pamoja na kusukutuwa na kuingiza maji puani.

**MAMBO MATANO AMBAYO NI WAJIBU KUOGA.**

1. Kutokwa na manii kwa njia ya ladha akiwa mtu yuko macho au akiwa usingizini kwa mwanamume au mwanamke, yatakapo toka manii bila ya matamanio kama vile yakitoka kwa sababu ya ugonjwa, au baridi kali hapaswi mtu kuoga, hivyo hivyo atakapoota na asipate manii au athari ya manii haitampasa kuoga pia, akipata manii au athari ya manii atawajibika kuoga hata kama hakumbuki kuwa aliota.
2. Kukutana kwa tupu mbili ya mwanamke na mwanamume kwa kuzamisha kichwa cha dhakari kwenye tupu ya mwanamke hata kama hayajatoka manii.
3. Kumalizika kwa hedhi na nifasi.
4. Mauti (kifo) ni wajibu maiti kuoshwa.
5. Atakapo silimu kafiri kuingia kwenye uislamu.

## MAMBO AMBAYO NI HARAMU KWA MWENYE JANABA.

Janaba ni neno ambalo linasifika kwa mwanamume na mwanamke pale wawili hawa watakapofanya tendo la ndoa, au kutoka na manii kwa matamanio bila ya tendo la ndoa au kutokwa na minii kwa sababu ya kuota.

Ni haramu kwa aliyepatwa na janaba;
1. Kuswali
2. Kutufu Al ka'aba
3. Kuugusa msahafu bila ya kizuizi, vile vile kuisoma Quran kwa siri au kwa wazi wazi, kwa hifidhi au kuisoma kawaida kwenye msahafu
4. Kukaa msikitini, ama kupita kwenye msikiti hakuna tatizo, na inafaa kukaa msikitini akitarajia kufanya hivyo, na itahafifisha kwa kutawadha.

## KUTAYAMAMU (KUJITWAHARISHA KWA KUTUMIA MCHANGA)

Inafaa kutayamamu ukiwa mjini au ukiwa safarini, kutayamamu inachukua nafasi ya uhu au kuoga itakapopatikanwa sababu miongoni mwa sababu zifuatazo;

1. Kukosekana maji, iwapo yatapatikana maji lakini hayatoshi kujitwaharishia, lakini inatakikana afanye juhudi za kuyatafuta kwanza, akiyakosa atatayamamu, au maji yanakuwa hayapo karibu yake, au anaogopea nafsi yake ikiwa atatawadha atadhurika, au mali yake kutokana na maudhi ya watu wabaya, asije akadhurika pindi akitoka nje kuyatafuta maji, hapo atatayamamu.
2. Ikiwa moja ya kiungo cha kutawadha kinajeraha, atakiosha na maji, na ikiwa kukiosha kwake kunaleta

athari basi atakipangusa na unyevu nyevu wa maji juu yake, ataulowesha mkono wake kisha ataupitisha juu ya hicho kiungo kilichokuwa na jeraha, na ikiwa kupangusa kunaathiri basi ataviosha baadhi ya viungo kisha kile chenye jeraha atakitayamamisha kwa mchanga.

3. Ikiwa maji ni ya baridi sana au hali ya hewa ni ya baridi sana na anaechelea kupata madhara pindi akitawadha kwa maji basi hapo atatayamamu.

4. Akiwa maji anayo, lakini anayahitajia kwa ajili ya kunywa au kupikia basi atatayamamu.

## NAMNA YA KUTAYAMAMU.

1. Atanuia moyoni mwake. (Kutia nia).

2. Atapiga viganja vyake viwili ardhini mara moja kisha atapangusa uso wake na kupangusa kwa kutumia matumbo ya vidole vyake, matumbo ya vidole vya mkono wa kushoto yatapangusa juu ya kiganja cha mkono wa kulia, na matumbo ya vidole vya mkono wa kulia yatapangusa juu ya kiganja cha mkono wa kushoto.

Inatenguka kutayamamu kwa yale yote yanayo tengua udhu, kama vile inatenguka kwa kupatikana maji kwa yule aliyekosa maji kabla ya swala au katikati ya swala, au atakaepata maji baada ya kumaliza kuswali, swala yake ni sahihi wala hawezi kuirudia swala yake.

# DAMU YA HEDHI NA NIFASI.

Damu ya Hedhi: Ni damu inyotoka katika hali ya afya ya mwanamke, inayotoka katika mfuko wa uzazi wa mwanamke sio kwa ajili ya kujifungua wala maradhi, katika muda maalumu, rangi yake ya kawaida ni nyesusi yenye harufu mbaya.

Damu ya Nifasi: Ni damu inayotoka kutoka kwenye mfuko wa uzazi wa mwanamke kwa sababu ya kujifungua.

Haifai kwa mwenye hedhi au Nifasi kusali au kufunga hali ya kuwa yupo kwenye Hedhi au Nifasi.

من حديث عائشة ـ رضي الله عنها ـ قالت: قال رسول الله ﷺ: ((إذا أقبلت الحيضة فدعي الصلاة، وإذا أدبرت فاغسلي عنك الدم وصلي)) [متفق عليه: ٣٣١]

Hadithi aliyoipokea mama Aisha mkewe Mtume (saw) anasema. amesema Mtume (saw): ("Itakapo kujia hedhi basi acha kusali, na itakapo ondoka, basi ioshe damu na usali") (Ameipokea Bukhari na Muslim:331, 333).

Hata zikidhi swala ambazo hajaziswali kipindi akiwa katika hali ya hedhi, isipokuwa swaumu atazilipa zile siku ambazo hajazifunga kutokana na hedhi au nifasi, kama vile ambavyo haifai kwa mwenye hedhi kutufu Al-Ka'aba, pia haifai mwanamume kumuingilia mwanamke akiwa katika hali ya hedhi, lakini inafaa kustarehe naye katika hali ya kuchezeana bila ya

kumuingilia, pia haifai kwa mwenye hedhi kuushika msahafu.

Atajitwaharisha mwenye hedhi kwa kukatika kwa damu ya hedhi, itamlazimu haraka kuoga ili aweze kujiondoa katika yale ambayo alikuwa amekatazwa kuyafanya.

Atakapo ingia hedhi mwanamke au kuwa na nifasi baada ya kuingia wakati wa swala kabla hajaswali, kauli sahihi ni kwamba atailipa hiyo swala baada ya kutwaharika na hedhi au nifasi.

Atakapo twaharika mwanamke kabla ya kutoka wakati wa swala kwa kiasi cha rakaa moja hivi, basi itamlazimu kuitekeleza swala hiyo, na inapendezwa azikidhi kwa kukusanya, mfano ikiwa ametwaharika kabla ya kuzama jua, basi itamlazimu aswali alasiri na inapendekezwa aikidhi swala ya adhuhuri, na ikiwa atatwaharika kabla ya nusu ya usiku basi ataiswali swala ya Ishai na inapendekezwa aikidhi swala ya magharibi.

# HUKMU ZA SWALA.

## أحكام الصلاة

Swala ni nguzo ya pili katika nguzo za uislamu, nayo ni wajibu juu ya kila muislamu baleghe mwenye akili timamu anawajibika kuitekeleza swala.

Awe amebaleghe kikamilifu kwa kufikia miaka kumi na tano kwa mwanaume, na awe ameshaanza kuota nywele za chini ya kinena (mavuzi) au ameshaanza kutokwa na manii kwa kuota au vinginevyo.

Kwa mwanamke ni kufikia umri wa miaka kumi na tano, kuota nywele za chini ya kinena, kutokwa na manii kwa njia ya kuota na kutokwa na hedhi, wakati anapotokewa mtu na vitu hizi basi atambue na kujua kuwa ameshabaleghe kafikia umri wa utu uzima.

Yeyote mwenye kupinga swala kwa makusudi basi atambue kuwa amekufuru kwa makubaliano ya wanavyuoni wote, au ikiwa ameicha swala kwa kuipuuza na uvivu basi kwa makubaliano ya maswahaba basi mtu huyo wamesema atakuwa amekufuru.

Swala ndio kitu cha kwanza akacho ulizwa mwanadamu siku ya kiyama kabla ya chochote kile mbele ya Allah.

Allah (sw) anasema:

﴿ إِنَّ الصَّلاةَ كَانَتْ عَلَى الْمُؤْمِنِينَ كِتَاباً مَوْقُوتاً ﴾ [النساء:١٠٣]

(Hakika ya swala kwa waumini ina wakati maalumu) (An-Nisai:103).

Hadithi ya Ibn Umar (R.A) bwana Mtume (asw) anasema:

عن ابن عمر رضي الله عنه، أن النبي -صلى الله عليه وسلم- قال: ((بُني الإسلام على خمس: شهادة إلا إله إلا الله، وأنَّ محمدًا رسول الله، وإقام الصلاة، وإيتاء الزكاة، والحج، وصوم رمضان)) [متفق عليه: ٨، ١٦ ]

((Uislamu umejengwa juu ya nguzo tano: Kushuhudulia ya kwamba hakuna mola anaepasa kuabudiwa kwa haki isipokuwa ni Mwenyezi Mungu pekee, na kushuhudia ya kuwa Muhammad ni Mtume wa Mwenyezi Mungu, na kusimamisha swala, na kutoa zaka, na kuhiji makkah, na kufunga mwezi wa Ramadhan)) ( Ameipoke Bukhar na Muslim: 8, 16).

Hadithi ya Jabir bin Abdillah (R.A) anasema:

وعن جابر بن عبدالله - رضي الله عنه - قال: سمعت رسول الله -صلى الله عليه وسلم- يقول: ((إنَّ بين الرجل وبين الشرك والكفر ترك الصلاة )) [رواه مسلم: ٨٢].

(Hakika tofauti iliyopo kati ya mtu, shirki na ukafiri ni kuiacha swala) (Ameipokea Imamu Muslim:82).

Hakika kutekeleza swala kuna fadhila kubwa sana, miongoni mwa fadhila hizo ni hadithi aliyoipokea Abu Huraira (R.A) amesema: Amesema Mtume (saw):

عن أبي هريرة ـ رضي الله عنه ـ قال: قال رسول الله ﷺ: ((من تطهر في بيته ثم مشى إلى بيت من بيوت الله، ليقضي فريضة من فرائض الله، كانت خطواته إحداهما تَحُطُّ خطيئة، والأخرى ترفع درجة )) [رواه مسلم: ٦٦٦]

(Mwenye kutawadha nyumbani kwake, kisha akatoka kuelekea nyumba miongoni mwa nyumba zake Allah, atakuwa kila hatua moja apigayo anafutiwa madhambi na hatu nyingine ananyanyuliwa daraja) (Ameipokea Imamu Muslim: 666).

وعنه رضي الله عنه ، أن رسول الله ـ صلى الله عليه وسلم ـ قال: ((ألا أدلكم على ما يمحو الله به الخطايا، ويرفع به الدرجات)) قالوا: بلى يا رسول الله، قال: ((إسباغ الوضوء على المكاره، وكثرة الخطا إلى المساجد، وانتظار الصلاة بعد الصلاة، فذلكم الرباط)) [رواه مسلم: ٢٥١ ].

(Hivi siwajulisheni kitu ambacho Allah anafuta madhambi kwa kitu hicho? Maswahaba wakamjibu kwanini usitulishe ewe Mjumbe wa Allah, Mtume akawaambia: (Nikuufanya vizuri udhu wako, na kuwa na hatua nyingi za kwenda msikitini, na kusubiri

swala baada swala nyingine, hiyo ndio ngome na ulinzi) (Ameipokea Imamu Muslim: 251)

وعنه - ﷺ - أيضًا، عن النبي -ﷺ- قال: ((من غدا إلى المسجد أو راح، أعد الله له في الجنة نزلاً، كلما غدا أو راح)) [ متفق عليه: ٦٦٢، ٦٦٩].

(Mwenye kwenda msikitini wakati wa asubuhi au wakati wa jioni Mwenyezi Mungu anamuandalia sehemu ya kufikia peponi, kila anapotoka asubuhi na jioni kwenda msikitini) ( Ameipokea Imamu Muslim: 662, 669).

**MAMBO MUHIMU YANAYOFUNGAMANA NA SWALA, NI HAYA YAFUATAYO;**

1. Uwajibu wa kswali jamaa msikitini kwa wanaume kutokana na Hadithi ya Mtume (saw) anasema:

(( لقد هممت أن آمر بالصلاة فتقام، ثم أخالف إلى منازل قوم لا يشهدون الصلاة معنا فأحرق عليهم )) [متفق عليه: ٢٤٢٠، ٦٥١].

(Ninanuia kuamrisha swala iswaliwe, kisha niondoke kwenda kwenye majumba ya watu ambao hawahudhurii swala msikitini nikayatie moto) (Ameipokea Bukhari na Muslim: 2420, 651).

2. Inatakiwa kwa muislamu kwenda msikitini mapema kwa utulivu na unyenyekevu.

3. Ni sunnah kwa yule mwenye kuingia msikitini atangulize mguu wa kulia, ataomba dua iliyopokelewa kwa Mtume (saw):

(( اللَّهُمَّ افْتَحْ لِي أَبْوَابَ رَحْمَتِكَ )) [ رواه مسلم: ١٦٥٢ ].

(Ewe mwenyezi mungu nakuomba unifungulie milango ya rehma zako) (Ameipokea Imam Muslim:1652).

4. Ni sunnah kuswali rakaa mbili tahiyat masjid (rakaa mbili za kusalimia msikiti) kabla ya kukaa, kwa hadithi aliyoipokea Abu Qatada (R.A):

لحديث أبي قتادة ﵁، أن رسول الله ﷺ قال: ((إذا دخل أحدكم المسجد، فليركع ركعتين قبل أن يجلس)) [متفق عليه: ٤٤٤، ٧١٤].

(Atakapo ingia mmoja wenu Msikitini aswali rakaa mbili kabla ya kukaa) (Ameipokea Bukhar na Muslim: 444, 714).

5. Ni wajibu kujisitiri tupu mbili wakati wa kuswali, na tupu ya mwanamume ni kuanzia kitivuni mpaka magotini na tupu ya mwanamke ni mwili wake wote ni uchi isipokuwa uso wake.

6. Ni wajibu kuelekea qibla, ni sharti la kukubaliwa swala, isipokuwa katika hali mbili;

A. Kupatikane kizuizi kutokana na maradhi na mfano wake, kikacho sababisha kutoweza kuelekea qibla.

B. Akiwa kwenye safari hali ya kuwa anakwenda hali ya kuwa kipando hakijaelekea Qibla, ataelekea kule kulikoelekea kipando, lakini kwenye swala za sunnah sio swala za faradhi.

7. Ni wajibu kutekeleza swala kwa wakati wake, kwani haiswihi swala kuswaliwa kabla ya wakati wake na haramu kuichelewesha swala kutoka kwenye wakati wake.

8. Kuleta takbira kwenye swala, na kupapia safu ya kwanza, na kusubiria swala, kufanya hivyo kuna fadhila kubwa sana.

Hadithi ya Abu Huraira: Mtume (saw) anasema:

فعن أبي هريرة ـ رضي الله عنه ـ قال: قال رسول الله ﷺ: ((لو يعلمُ الناس ما في النداء والصف الأول، ثم لم يجدوا إلا أن يستهموا عليه لاستهموا، ولو يعلمون ما في التهجير [ أي: التبكير] لاستبقوا إليه ... الحديث)) [ متفق عليه: ٦١٥، ٤٣٧ ].

(Laiti watu wangelijua ubora wa adhana na swafu ya kwanza, kisha wasipatikane isipokuwa kwa kutoa kitu wangelitoa, na laiti watu wangelijua ubora wa takbira ya pamoja na Imamu wangeishindania...) (Ameipokea Bukhar na Muslim:615, 437).

وعنه رضي الله عنه، أَن رسول الله ـ ﷺ ـ قال: ((لا يزالُ أحدُكُم فِي صلاةٍ ما دامت الصلاةُ تَحبِسهُ...الحديث )) [رواه البخاري ومسلم: ٦٥٩ - ٦٤٩].

(Hataacha kuwa mmoja wenu kwenye swala maadamu swala inamzuiya) (Ameipokea Bukhar na Muslim: 659, 649).

## NYAKATI ZA SWALA.

1. Wakati wa swala ya adhuhuri ni kuanzia kumili jua kuelekea upande wa magharibi mpaka kitakapo kuwa kuvuli kinalingana sawa mfano wake kwa urefu.

2. Wakati wa swala ya alasiri ni kuanzia kinapolinga sawa kivuli mfano wake mpaka kuzama kwa jua.

3. Wakati wa swala ya magharibi ni kuanzia kuzama kwa jua mpaka kupotea kwa mawingu mekundu, nao ni wekundu unaojitokeza wakati wa kuzama kwa jua.

4. Wakati wa swala ya Ishai ni kuanzia yanapopotea mawingu mekundu mpaka nusu ya usiku.

5. Wakati wa swla ya alfajir ni kuanzia kuchomoza kwa alfajiri mpaka kuchomoza kwa jua.

## SEHEMU AMBAZO HAZIFAI KUSWALI NDANI YAKE.

Sehemu ambazo hazifai kuswali ndani yake ni;

1. Makaburini kwa kauli yake Mtume (saw) aliposema:

((الأرض كلها مسجدٌ، إلا الحمَّام والمقبرة)) [ رواه الخمسة، وهو حديث صحيح]

(Ardhi yote ni msikiti, isipokuwa chooni na makaburini) (Imepokelewa na wapokezi watano nayo ni hadithi sahihi).

Ama swala ya jenenza inafaa kuswaliwa makaburini bila ya tatizo lolote kwani haina rukuu wala kusujudu, lakini swala za kawaida haifai kuswali makaburini.

2. Kuswali kuelekea makaburini, kutokana na hadithi Abu Marthad Alghanawiy (R.A) anasema, alimsikia Mtume (saw) akisema:

فعن أبي مَرثَد الغَنَوي ـ رضي الله عنه ـ قال: سمعت رسول الله ـ صلى الله عليه وسلم ـ يقول: ((لا تصلوا إلى القبور، ولا تجلسوا عليها )) [رواه مسلم: ٩٧٣].

(Msiswali kuelekea makaburini, wala msikae juu ya makaburi) (Ameipokea Imamu Muslim: 973).

3. Kuswali kwenye zizi la ngamia, kama vile haifai kuswali sehemu ambazo kuna najisi.

# NAMNA YA KUSWALI.

Ukitaka kuswali ni lazima uhudhurishe nia yako wakati wa kuswali, na hiyo ni katika ibada zote anazotaka mtu kuzifanya, na nia inakuwa moyoni bila ya kuitamka kwa ulimi.

Namna ya kuswali ni kama ifuatavyo;
1. Kwanza ni kuelekea qiblah mwili wake wote sio kupinda wala kugeuka geuka.

2. Kisha kupiga takbira ya kuhirimia swala atasema (الله أكبر) Allahu Akbar huku akinyanyua mikono yake karibia na mabega yake au karibia na masikio yake wakati wa kuileta takbira.

3. Kisha ataweka kiganja chake cha kulia juu ya kiganja chake cha kushoto juu ya kifua chake.

4. Kisha ataisoma dua ya kufungua swala ambayo ni;

((الحَمْدُ لله حَمْدًا كَثِيرًا طَيِّبًا مُبَارَكًا فِيهِ)) [رواه مسلم: ٦٠٠].

أو: ((سُبْحَانَكَ اللَّهُمَّ وَبِحَمْدِكَ، وَتَبَارَكَ اسْمُكَ، وتَعَالَى جَدُّكَ، وَلاَ إِلَهَ غَيْرُكَ)) [رواه أبو داود والترمذي:٧٧٥، ٢٤٢. وصححه الألباني]

Au ataisoma dua yoyote katika dua za kufungulia swala, na ni bora kusoma dua mbali mbali katika dua za kufungulia swali mtu asidumu na dua moja kila wakati hiyo inapelekea unyenyekevu na kuhudhurisha moyo.

5. Kisha atasema AUDHU BILLAH MINA SHAITWANI RAJIIM

(أعوذ بالله من الشيطان الرجيم)

6. Kisha atasema:

(بسم الله الرحمن الرحيم)

Kisha atasoma surat Fatiha (Alhamdu lillah) mpaka mwisho na atasema Ameena آمين

7. Kisha atasoma anachoweza katika Quran sura yoyote.

8. Kisha atanyanyua mikono yake karibia na mabega yake wakati wa kurukuu atasema Allahu Akbar, na katika kurukuu ataiweka mikono yake kwenye magoti yake akiwa amevipanua vidole vyake sio kuvibana akisema kwenye rukuu (SUBHANA RABBIYAL ADHWIMU) mara tatu, na inafaa kusema zaidi ya mara tatu, hata akisema mara moja hakuna shaka.

9. Kisha atanyanyua kichwa chake kutoka kwenye kurukuu akisema:
(SAMI'A LLAHU LIMAN HAMIDAH) kwa Imamu na maamuma wote watasema hivyo, hali ya kunyanyua

mikono karibia na mabega wakati wa kunyanyuka kutoka kurukuu, Imamu na Maamuma wote watasema hivyo:

(RABBANA WALAKAL HAMD) badala ya kusema (SAMI'A LLAHU LIMAN HAMIDH), ataweka kiganja chake cha kulia juu ya kiganja chake cha kushoto juu ya kifua chake. (Atairudisha mikono yake kifuani).

10. Atasema wakati akiwa amesimama:

(( اللَّهُمَّ رَبَّنا لَكَ الحَمْدُ، مِلْءَ السَّمَاوَاتِ ومِلْءَ الأَرْضِ وَمِلْءَ مَا بينَهُما، وَمِلْءَ مَا شِئْتَ مِنْ شَيْءٍ بَعْدُ )) [ رواه مسلم: ٧٧١ ].

11. Kisha atasujudu sijda ya kwanza na atasema wakati wa kusujudu Allahu Akbar, visujudu viungo vyake vyote saba ambavyo ni uso pamoja na pua, viganja viwili, magoti mawili, vidole vya miguu miwili, atajiepusha kuibana mikono yake kwenye mbavu, na ataelekeza vidole vya miguu yake kuelekea qiblah, huku akisema katika kusujudu: (SUBHANA RABBIYAL A'ALA) mara tatu au zaidi ya hiyo au hata mara moja inafaa.

Lakini inapendeza kuzidisha dua kwenye sijda ni sehemu za kupokelewa dua kwa haraka.

12. Kisha atanyanyua kichwa chake kutoka kusujudu akisema Allahu Akbar na atakaa kati ya sijida mbili akikalia mguu wake wa kushoto na akisimamisha mguu wake wa kulia na akiweka mkono wake wa kushoto juu ya paja lake la kushoto na hali ya kuwa vidole vya mkono wake amevifumba pamoja, na atasema wakati akiwa amekaa: (RABBI IGHFIRLII, RABBI IGHFIRLII)

13. Kisha atasujudu mara ya pili atafanya kama alivyofanya kwenye sijida ya kwanza.

14. Kisha atasimama kutoka sijida ya pili akisema ALLAHU AKBAR na atasimama wima (kuitadili).

15. Kisha ataswali rakaa ya pili kama alivyofanya na kusema kwenye rakaa ya kwanza, lakini hatasoma dua ya kufungulia swala wala kusema A'AUDHU BILLAH, baada ya kusujudu rakaa ya pili atakaa kama alivyokaa kati ya sijida mbili, isipokuwa atavifunga vidole vyake vya mkono wa kulia atalifunga dole gumba na kidole cha shahada na akiashiria kwa kidole cha shahada atasoma Tashahudi (Tahiyyatu) kwenye kikao hicho, na Tashahudi ni kusoma:

((التَّحِيَّاتُ لله، والصَّلَوَاتُ والطيِّبَاتُ، السَّلاَمُ عَلَيْكَ أيُّهَا النبيُّ وَرَحْمَةُ الله وبَرَكَاتُهُ، السَّلاَمُ عَلَيْنَا وعَلَى عِبَادِ الله الصَّالِحِينَ، أَشْهَدُ أَنْ لا إلهَ إلا الله، وأَشْهَدُ أَنَّ مُحَمَّداً عَبْدُهُ ورَسُولُهُ)) [ رواه البخاري: ٨٣١ ].

Tahiyyatu imepokewa katika mapokezi aina nyingi sana, ni vizuri mtu ukajifunza na kuielewa.
Kisha atasimama ikiwa anaswali swala yenye rakaa tatu kama swala ya magaribi, au swala yenye rakaa nne kama swala ya adhuhuri au alasiri na Ishai akisema: ALLAHU AKBAR akinyanyua mikono yake karibia na mabega yake wakati wa kunyanyuka, kisha atakamilisha rakaa zilizobakia kwenye swala yake, kama namna alivyofanya kwenye rakaa ya pili, isipokuwa atasoma surat fatiha pekee wakati wa kusimama.

Na baada ya kusujudu sijida ya pili kutoka rakaa ya mwisho atakaa na kusoma tashahudi (Tahiyyatu ya mwisho) na kumswalia Mtume Swalallahu A'alayhi Wasallam katika swalat Ibrahimiyya.


((التَّحِيَّاتُ لله، والصَّلَوَاتُ والطيِّبَاتُ، السَّلاَمُ عَلَيْكَ أَيُّهَا النبيُّ وَرَحْمَةُ الله وبَرَكَاتُهُ، السَّلاَمُ عَلَيْنَا وعَلَى عِبَادِ الله الصَّالِحِينَ، أَشْهَدُ أَنْ لا إلهَ إلا الله، وأَشْهَدُ أَنَّ مُحَمَّداً عَبْدُهُ ورَسُولُهُ، اللّهُمَّ صَلِّ عَلَى مُحَمَّدٍ، وَعَلَى آلِ مُحَمَّدٍ، كما صَلَّيْتَ عَلَى إبراهيم وَعَلَى آلِ إبْرَاهيمَ، إنَّكَ حَمِيدٌ مَجِيدٌ، اللهم بَارِكْ عَلَى مُحَمَّدٍ، وعَلَى آلِ مُحَمَّدٍ، كَمَا بَارَكْتَ عَلَى إبْرَاهيمَ، وَعَلَى آلِ إبْرَاهيمَ، إنَّكَ حَمِيدٌ مَجِيدٌ)).

Kisha baada ya hapo ataomba dua yoyote atakayo, lakini ni sunnah kufanya wingi katika kuomba dua, ni vizuri aombe dua ilikuja katika mafundisho ya Mtume (saw):

((اللَّهُمَّ إِنِّي أَعُوذُ بِكَ مِنْ عَذَابِ الْقَبْرِ، وَمِنْ عَذَابِ النَّارِ، وَمِنْ فِتْنَةِ المَحْيَا والمَمَاتِ، ومِنْ فِتْنَةِ المَسِيحِ الدَّجَّالِ)).

16. Kisha atatoa salamu upande wa kulia kwa kusema: "ASSALAAMU A'LAYKUM WARAHMATULLAH" na upande wa kushoto hivyo hivyo.

17. Ni sunnah katika Tahiyyatu ya mwisho kwenye swala ya adhuhuri, Alasiri, magharibi na Ishai akae mwenye kuswali kikao cha kulaza mguu wa kushoto kisha akisimamisha mguu wa kulia autoe mguu wake wa kushoto kupitia kwenye chini ya muhundi wake wa kulia, huku akiyaambatanisha makalio yake na ardhi, na ataweka mikono kwenye mapaja kama alivyofanya kwenye Tahiyyatu ya kwanza.



## ADHKARI BAADA YA SWALA. (NYIRADI BAADA SWALA)

Inapendeza kwa mwenye kuswali aseme hizi adhkari baada ya kumaliza swala ya faradhi;

((أَسْـتَغْفِرُ الله، أَسْـتَغْفِرُ الله، أَسْـتَغْفِرُ الله، اللَّهمَ أَنْتَ السَّـلامُ ومِنْكَ السَّلامُ، تَبَارَكتَ يا ذَا الجَلالِ والإِكْرَام)) [ رواه مسلم: ٥٩١ ].

Aseme: Astaghfiru Allah, Astaghfiru Allah, Astaghfiru Allah, Allahumma Antassalaamu wamikassalaamu, tabarakta yaa dhal jalaal walikrami.

Maana ya maneno haya: ((Namuomba Mwenyezi Mungu Msamaha, Namuomba Mwenyezi Mungu Msamaha, Namuomba Mwenyezi Mungu Msamaha, hakika yako Mwenyezi mungu wewe ni Amani na kwako ndiko kwenye Amani, na umetukuka ewe mwenye utukufu na ukarimu)) (Ameipokea Muslim: 591)

Ataisoma na dhikri hii:

((لاَ إِلهَ إِلاَّ اللهُ وَحْدَهُ لاَ شَرِيكَ لَهُ، لَهُ المُلْكُ، وَلَهُ الحَمْدُ، وَهُوَ عَلى كُلِّ شَيءٍ قَديرٌ، اللَّهمَ لاَ مَانِعَ لِما أَعْطَيتَ، ولاَ مُعْطِيَ لِما مَنَعْتَ، ولاَ يَنْفَعُ ذا الجِدِّ مِنْكَ الجَد)) [ متفق عليه: ٨٤٤، ٥٩٣].

((Hapana mola apasae kuabudiwa kwa haki isipokuwa Mwenyezi Mungu pekee asiekuwa na mshirika, Mwenye Ufalme, Mwenye kuhimidiwa na yeye juu ya kila kitu ni muweza, Ewe Mola wangu hakuna Mwenye kuzuia yule uliye mpatia, na walahapewi yule uliemnyima, na wala hatonufaika kwako mwenye cheo kwa cheo chake.)) (Ameipokea Bukhar na Muslim: 844,593)

((لاَ إِلهَ إِلاَّ اللهُ وَحْدَهُ لاَ شَـــرِيكَ لَهُ، لَهُ الْمُلْكُ، وَلَهُ الحَمْـــدُ، وَهُوَ عَلى كُلِّ شَيءٍ قَديرٌ، لاَ حَوْلَ وَلاَ قُوَّةَ إِلاَّ بِالله، لاَ إِلهَ إِلاَّ اللهُ، ولاَ نَعبُدُ إِلاَ إِيَّاهُ، لهُ النِّعمَةُ ولهُ الفَضْـلُ، ولهُ الثنَاءُ الحَسَـنُ، لاَ إِلهُ إِلاَّ اللهُ مُـخْلِصينَ لهُ الدِّينَ ولَو كَرِهَ الكَافِرونَ )) [ رواه مسلم: ٥٩٤].

((Hakuna mola apasae kuabudiwa kwa hakiisipokuwa ni Mwenye Mungu pekee, Mwenye ufalme, Mwenye kuhimidiwa na kusifiwa, na yeye juu ya kila kitu ni muweza, hakuna hila wala nguvu za aina yoyote isipokuwa ni zake Mwenyezi Mungu, hapana mola apasae kuabudiwa kwa haki isipokuwa yeye, hatumuabudu yeyote isipokuwa yeye, anazo neema mbali mbali na fadhila na yeye ndiye mwenye sifa nzuri, hapana mola apasae kuabudiwa kwa haki isipokuwa ni Mwenyezi Mungu, tunamtakasia yeye dini hata kama watachukia makafiri )) (Ameipokea Muslim:594)

بعدها يقول: ((سُـــبْحَانَ الله)) ثلاثًا وثلاثين مرةً، و ((الحَمْدُ الله)) ثلاثًا وثـلاثين مرةً ، و (( اللهُ أَكْــبَر )) ثـلاثـا وثلاثين مرةً.

Baada ya hizi adhkari atasema: SUBHANALLAH mara 33, ALHAMDULILLAH mara 33 na ALLAHU AKBAR mara 33.

ثم يقول تمام المئة: (( لاَ إلهَ إلاَّ اللهُ وَحْدَهُ لاَ شَرِيكَ لَهُ، لَهُ المُلْكُ، وَلَهُ الحَمْدُ، وَهُوَ عَلَى كُلِّ شَيءٍ قَديرٌ )) . [ رواه مسلم: ٥٩٧].

Kisha atasema kwa kukamilisha mia moja: LAAILAAHA ILLA ALLAH WAHDAHU LAA SHARIIKALAHU LAHULMULKU WALAHUL HAMDU WAHUWA A'ALAA KULLI SHAIN QADIIR. (Ameipokea Muslim: 597)

((Atasema: Hapana mola apasae kuabudiwa kwa haki isipokuwa ni Mwenyezi Mungu mmoja tu asiekuwa na mshirika, Mwenye Ufalme na Mwenye kuhimidiwa na yeye juu ya kila kitu ni muweza.)) (Ameipokea Muslim: 597)

ويقرأ آية الكرسي، وقل هو الله أحد، وقل أعوذ برب الفلق، وقل أعوذ برب الناس بعد كل صلاة، ويستحب تكرار هذه السور الثلاث، ثلاث مراتٍ بعد صلاة الفجر والمغرب.

Na atasoma ayat kursiy, atasoma surat Ikhlas (kul huwallahu), atasoma Surat falaq na Surat Nnas atazisoma kila baada ya swala.

Na inapendeza kama atazisoma hizo sura kwa kuzirudia rudia mara tatu tatu baada ya swala ya alfajir na swala ya maghribi.

## ALIETANGULIWA KATIKA SWALA.

Alietanguliwa katika swala ni yule ambae ilimpita rakaa au zaidi ya rakaa ndani ya swala, na akasimama kukamili zile ambazo zilimpita baada ya Imamu kutoa salamu ya pili ya kumaliza swala, atakuwa ni mwenye kuipata rakaa pale atakapo mdiriki Imamu kwenye rukuu, ama akiwa hatamdiriki Imamu kwenye rukuu basi itakuwa ameikosa rakaa pamoja na Imamu na itakuwa rakaa hiyo imempita.

Na inatakiwa kwa alietanguliwa anapoingia msikitini moja kwa moja akajiunge kwenye swala ya jamaa popote atakapo mkuta imamu ndani ya swala, sawa sawa amkute Imamu amesimama au amerukuu, amesujudu au popote pale yeye anatakiwa kuunga jamaa, haitakikani kusubiri mpaka Imamu aanze rakaa ya pili ndipo aunge naye sivyo, bali ataleta takbira ya kuhirimia swala kisha moja kwa moja

ataunga swala pale alipomkuta Imamu isipokuwa kwa mwenye udhuru kama vile mgonjwa.

## VYENYE KUBATILISHA SWALA.

1. Kuzungumza kwa makusudi hata kama maneno ni kidogo.
2. Kutoelekea qibla mwili wako wote.
3. Kutokea kitenguzi miongoni mwa vitengua udhu.
4. Kufanya harakati nyingi kwa kufuatana isipokuwa kwa dharura.
5. Kucheka ndani ya swala hata kama ni kidogo.
6. Atakapo zidisha rakaa, kusujudu, kisimamo au kikao kwa makusudi kufanya hivyo.
7. Kumtangulia Imamu kwa makusudi.

## MAMBO YA WAJIBU KWENYE SWALA.

1. Takbira zote isipokuwa takbira ya kuhirimia swala.
2. Kusema SUBHANA RABBIYAL ADHWIMU mara moja.
3. Kusema SIMI’ALLAHU LIMAN HAMIDA kwa Imamu na kwa mtu pekee, wakati wa kunyanyuka kutoka kurukuu.

4. Kusema RABBANA WALAKAL HAMDU baada ya kutoka kurukuu.
5. Kusema SUBHANA RABBIYAL A’ALA mara moja katika kusujudu.
6. Kusema RABBIGHFIRILII kati ya sijida mbili.
7. Tahiyyatu ya kwanza.
8. Kikao cha tahiyyatu ya kwanza.

## NGUZO ZA SWALA.

1. Kusimama pamoja na uwezo kwenye swala za faradhi, kwa swala za sunnah sio lazima kusimama, lakini kuswali kwa kukaa ina ujira wa nusu kuliko yule mwenye kuswali kusimama
2. Takbira ya kuhirimia swala.
3. Kusoma surat fatiha katika kila rakaa.
4. Kurukuu kwa kila rakaa.
5. Kuitadili kutoka kurukuu kwa kusimama wima.
6. Kusujudu kwa viungo saba mara mbili kwa kila rakaa.
7. Kukaa kati ya sijda mbili.
8. Kujituliza katika vitendo vyote tulivyo vitaja hapo juu.
9. Tahiyyatu ya mwisho.
10. Kitako cha tahiyyatu ya mwisho.

11. Kumswalia Mtume (saw).
12. Kutoa salamu.
13. kufuata mpangilio kwa kila nguzo.

## KUSAHAU KWENYE SWALA.

Atakapo sahau mwenye kuswali ndani ya swala yake, kwa kuzidisha au kupunguza, au akapatwa na shaka kuwa amezidisha au amepunguza, itamuwajibika kusujudu sijdatu sahawi (sijda ya kusahu).

Ikiwa atazidisha chochote kwenye swala kwa kusahau akazidisha kisimamo, kurukuu, kitako au mfano wa hayo hapo atasujudu sijda ya kusahau sijida mbili baada ya salamu.

Na hivyo hivyo atakapo punguza kwenye swala yake kwa kuacha chochote miongoni mwa vitendo vya swala au katika maneno ya swala, ikiwa alicho kiacha ni nguzo, basi akikumbuka kabla ya kulazimika kusoma rakaa inayofuata, atarudi na kuileta ile nguzo aliyoiacha, kisha atasujudu sijda ya kusahau.

Ikiwa atakumbuka baada ya kuingia rakaa ifuatayo, basi itabatilika rakaa ambayo aliiacha, na itachua nafasi yake rakaa ambayo anaisali, ile ya nyuma itakuwa haipo.

Ikiwa hataijua nguzo aliyoiacha ni ipi baada ya salamu, ikiwa hakuna kitambo kidogo basi ataileta nguzo kamili na atasujudu sijda ya kusahau, lakini kukiwa na kitambo kidogo au udhu wake ukatenguka, atairudia swala yake upya.

Ikiwa atakuwa amesahu kufanya jambo la wajibu katika swala mfano wa kukaa kitako cha Tahiyyatu ya kwanza au mfano wake katika wajibati za swala, atasujudu sijida mbili kabla ya kutoa salamu.

Ama katika hali ya shaka, akawa na shaka katika idadi ya rakaa alizoswali hajui kaswali rakaa ngapi kaswali mbili au tatu, hapo atajengea juu ya uchache kuwa ameswali rakaa mbili, kwani mwenye kuwa na yakini atasujudu sijida ya kusahau kabla ya salamu.

Akiwa na shaka kuwa ameacha nguzo ataileta ile nguzo aliyoiacha na nguzo iliyopo, kisha atasujudu sijda ya kusahau.

## SUNNAH ZINAZO AMBATANA NA SWALA ZA FARADHI. (RAWATIBU).

Inapendekezwa kwa kila muislamu wa kike na wakiume, azihifadhi na kudumu nazo rakaa kumi na mbili za sunnah akiwa sio msafiri.

Rakaa mbili hizo ni rakaa nne kabla ya adhuhuri, rakaa mbili baada ya adhuhuri, rakaa mbili baada ya

magharibi, rakaa mbili baada ya Ishai na rakaa mbili kabla ya swala ya alfajir.

فعن أم حبيبة -رضي الله عنها- قالت: سمعت رسول الله -صلى الله عليه وسلم- يقول: (( مَا مِنْ عَبْدٍ مُسْلِمٍ يُصَلِّي لِلَّهِ كُلَّ يَوْمٍ ثِنْتَيْ عَشْرَةَ رَكْعَةً تَطَوُّعًا غَيْرَ فَرِيضَةٍ إِلَّا بَنَى اللَّهُ لَهُ بَيْتًا فِي الْجَنَّةِ، أَوْ إِلَّا بُنِيَ لَهُ بَيْتٌ فِي الْجَنَّةِ )) [رواه مسلم: ٧٢٨].

(Hakuna mja yeyote muislamu mwenye kuswali kila siku rakaa kumi na mbili za sunnah, isipokuwa Allah atamjengea nyumba peponi, au atajengewa nyumba peponi) (Ameipokea Imamu Muslim: 728).

Ni vyema kuswali hizi sunnah za rawatibu zinazo ambatana na swala za faradhi kuswaliwa msikitini, ama sunnah nyinginezo ni vizuri ziswaliwa nyumbani.

فعن جابر بن عبدالله -رضي الله عنه- قال: قال رسول الله -صلى الله عليه وسلم-: ((إذا قضى أحدكم الصلاة في مسجده، فليجعل لبيته نصيبًا من صلاته، فإن الله جاعلٌ في بيته من صلاته خيرًا)) [رواه مسلم: ٧٧٨]

(Atakapo maliza mmoja wenu swala yake msikitini, basi ajaalie nyumbani kwake sehemu ya swala yake, kwa hakika ya Mwenyezi Mungu anaweka kheri ya haraka kwenye nyumba yake kutokana na swala yake ya sunnah aliyoisali nyumbani.) (Ameipokea Imamu Muslim:778).

عن زيد بن ثابت ـ رضي الله عنه ـ قوله ﷺ: (( ... فإنَّ خير صلاة المرء في بيته، إلا الصلاة المكتوبة ))[ متفق عليه: ٦١١٣، ٧٨١ ].

(Hakika ya swala bora anayoiswali mtu, ni lie swala anayoiswali nyumbani kwake isipokuwa swala ya faradhi) (Ameipokea Bukhar na Muslim:6113, 781).

## SWALA YA WITRI.

Inasuniwa kwa muislamu kuitekeleza swala ya witri, nayo ni sunnah iliyosisitizwa sana, na wakati wake wa kuiswali ni kuanzia baada ya swala ya Ishai mpaka kuchomoza Alfajir, na wakati wake mzuri kuiswali ni mwisho wa usiku kwa yule mwenye yakini ya kuamka usiku huo, swala hii ni miongoni mwa sunnah ambazo Mtume (saw) hakuiacha bali alikuwa akidumu nayo kwenye safari na hata akiwa hasafiri, na uchache wa rakaa zake ni rakaa moja.

Na alikuwa Mtume wa Allah akiswali usiku rakaa kumi na moja, kama ilivyopokewa Hadithi ya mama Aisha (R.A):

عن عائشة رضي الله عنها: ((أن رسول الله ـ ﷺ ـ كان يصلي بالليل إحدى عشرة ركعة، يوتر منها بواحدة ... الحديث ))[رواه مسلم:٧٣٦]

(Hakika Mtume wa Allah alikuwa akiswali swala za usiku rakaa kumi na moja, na akiswali witri rakaa moja) (Ameipokea Imamu Muslim:736).

Swala za usiku ni rakaa mbili mbili kama ilivyokuja kwenye hadithi ya Ibn Umar (R.A) kwamba kuna bwana mmoja alikuja kwa Mtume (saw) akimuuliza kuhusu swala za usiku Mtume akamjibu swala za usiku za sunnah ni rakaa mbili mbili:

عن ابن عمر ﵁، أن رجلاً سأل رسول الله -ﷺ- عن صلاة الليل، فقال رسول الله ﷺ: ((صلاة الليل مثنى مثنى، فإذا خشي أحدكم الصبح، صلى ركعة واحدة، توتر له ما قد صلى)) [رواه مسلم: ٧٤٩].

(Mtume amesema: (Swala ya usiku ni rakaa mbili mbili, basi akiechelea mmoja wetu kuwa asubuhi itampita, ataswali rakaa moja, na ataandikiwa kuwa ameswali swala ya witri) (Ameipokea Imamu Muslim: 849).

Inapendekezwa mara nyingine akunuti baada ya kurukuu katika swala ya witri, kwa Hadithi ya Hassan bin Alliy (R.A) pale ambapo Mtume (saw) alimfundisha maneno ayaseme katika dua ya swala ya Witri, lakini asidumu nayo.

Kwa hakika wengi wa wanavyuoni walioelezea swala ya Mtume (saw) hawakutaja kunuti yake Mtume (saw).

Kama inavyopendekezwa kwa yule ambae imempita swala ya usiku anaweza kuikidhi mchana kwa kuswali rakaa mbili, rakaa nne, rakaa sita, rakaa nane, rakaa kumi au rakaa kumi na mbili kwa kufuata alivyofanya Mtume (saw).

## RAKAA MBILI ZA ALFAJIRI.

Miongoni wa sunnah zinazo ambatana na swala za faradhi alizokuwa Mtume (saw) akidumu nazo akiwa safari au akiwa hayuko safari ni rakaa mbili kabla ya alfajiri.

عن عائشة رضي الله عنها: ((أن النبي - صلى الله عليه وسلم - لم يكن على شيء من النوافل، أشد معاهدة منه، على ركعتين قبل الصبح )) [متفق عليه: ١١٦٣، ٧٢٤]

(Hadithi aliyoipokea Mama Aisha (R.A) anasema: Hakika ya Mtume (saw) hakuwa na kitu chochote katika sunnah alichofungamana nacho, zaidi ya rakaa mbili za sunnah kabla ya swala ya subhi) (Ameipokea Imamu Muslim: 1163, 724).

ولقوله - صلى الله عليه وسلم -: (( لهما أحبَّ إليَّ من الدنيا جميعًا )) [رواه مسلم: ٧٢٥].

(Na kauli yake Mtume katika kuzizungumzia rakaa mbili hizi: (Ya kwamba ninazipenda zaidi kuliko dunia yote) (Ameipokea Imamu Muslim: 725).

Ni sunnah unaziswali rakaa mbili hizi kusoma rakaa ya kwanza Surat Fatihah na Surat Kafiruna ( قل يأيها الكافرون) na rakaa ya pili Surat Fatihah (قل هو الله أحد) mara nyingine anaweza kusoma rakaa ya kwanza

(قُولُوا آمَنَّا بالله وَمَا أُنزِلَ إِلَينَا ... الآية )

na katika rakaa ya pili ataisoma ayah hii:

(قُل يا أهل الكتاب تَعَالَوا إلى كلمةٍ سَوَاءٍ بيننا وبينكم... )

Kama ilivyo sunishwa kuziswali kwa kuzihafifisha, kwa alivyofanya Mtume (saw) na inafaa kwa yule aliyepitwa na hizi rakaa mbili za kabla ya alfajir, atazikidhi baada ya swala, na ni bora azikidhi kabla ya kuchomoza kwa jua na liwe liko kiasi cha urefu wa mkuki mpaka kufikia kabla ya wakati wa makatazo muda wa kuwa jua kumili.

## SWALA YA DHUHA.

Nayo ni swala ya wenye kurejea kwa Allah (sw) (wenye kutubia), ni sunnah iliyosisitizwa zimepokelewa hadithi nyingi za kutilia mkazo juu ya swala hii.

Hadithi ya Abu Dharri (R.A) Mtume (saw) anasema:

عن أبي ذر ﵁، عن النبي -ﷺ- أنه قال: ((يُصبحُ على كل سلامى (أي: مفصل) من أحدكم صدقة، فكل تسبيحة صدقة، وكل تحميدة صدقة، وكل

تهليلة صدقة، وكل تكبيرة صدقة، وأمر بالمعروف صدقة، ونهي عن المنكر صدقة، ويجزىء من ذلك ركعتان يركعهما من الضحى)) [ رواه مسلم: ٧٢٠ ]

(Mtume (saw) anasema: Kinapambaukiwa kila kiungo cha mmoja wenu kuwa ni swadaka, kila tasbihi ni sadaka, na kila tahmiid ni swadaka, na kila tahlilu ni swadaka, na kila takbira ni swadaka, na kuamrisha mema ni swadaka, na kukataza maovu ni swadaka, na inalipwa kutokana na hayo rakaa mbili anazoziswali za Dhuha) (Ameipokea Imamu Muslim: 820).

وعن أبي هريرة - ﷺ - قال: ((أوصاني خليلي بثلاث، لا أدعهن حتى أموت: صوم ثلاثة أيام من كل شهر، وصلاة الضحى، ونوم على وتر )) [ متفق عليه: ١١٧٨، ٧٢١ ].

(Hadithi ya Abu Huraira (R.A) anasema: (Ameniusia kipenzi changu mambo matatu nisiachane nayo mpaka nife, ameniusia kufunga siku tatu za kila mwezi, na swala ya Dhuha na kulala nikiwa nimeswali swala ya witri) (Ameipokea Bukhar na Muslim: 1178 , 721).

Wakati mzuri wa kuiswali swala ya Dhuha ni pale jua litakapo nyanyuka kiasi cha mkuki, na jua likawa linachoma, na wakati wake unatoka pindi jua litakapo mili upande wa magharibi, na uchache wa rakaa zake ni rakaa mbili na wala aina kiwango maalum.

## NYAKATI ZILIZO KATAZWA KUSWALI.

Kuna nyakati ambazo zimekatazwa kuswali ndani ya nyakati hizo;

1. Baada ya swala ya alfajir mpaka kuchomoza kwa jua lifike kiasi cha mkuki.

2. Wakati jua likiwa katikati wakati wa mchana mpaka limili upande wa magharibi.

3. Baada ya swala ya alasir mpaka kuzama kwa jua.

Lakini inafaa kutekeleza baadhi ya swala katika nyakati hizi zilizokatazwa mfano swala zenye sababu maalumu kama vile Tahiyyatul masjid (sunnah ya kuingia msikitini), swala ya jeneza, swala ya kupatwa kwa jua, rakaa mbili za twawafu, rakaa mbili za udhu na mfano wake.

Vile vile inafaa kukidhi swala za faradhi zilimpita mtu kwenye nyakati hizi, Mtume (saw) anasema:

لقوله ﷺ: ((من نسي صلاةً أو نام عنها، فكفارتها أن يُصليها إذا ذكرها)) [متفق عليه:٥٩٧، ٦٨٤]

(Mtume (saw) anasema: Mwenye kuisahau swala au akalala, basi kafara lake ni kuiswali hiyo swala pindi atakapo ikumbuka) (Ameipokea Imamu Bukhar na Muslim:597, 684).

Kadhalika anaweza kuikidhi sunnah ya alfajir zile rakaa mbili kabla ya alfajir zikiwa zimempita katika kuzitekeleza kwa wakati wake.

# FIHRISI YA KITABU

HUKMU ZA TWAHARA.....3
TWAHARA NA NAJISI.....3
AINA ZA NAJISI.....5
MIONGONI WA HUKUMU ZA NAJISI.....6
KUKIDHI HAJA.....6
UDHU.....8
NAMNA YA KUTAWADHA.....9
KUPANGUSA KHOFU MBILI.....12
VYENYE KUTENGUA UDHU.....13
KUOGA (JOSHO).....13
MAMBO AMBAYO NI HARAMU KWA MWENYE JANABA. 14
KUTAYAMAMU.....15
NAMNA YA KUTAYAMAMU.....16
DAMU YA HEDHI NA NIFASI.....17
HUKMU ZA SWALA.....19
NYAKATI ZA SWALA.....25
SEHEMU AMBAZO HAZIFAI KUSWALI NDANI YAKE.....26
ADHKARI BAADA YA SWALA.(NYIRADI BAADA SWALA) 33
ALIETANGULIWA KATIKA SWALA.....36
VYENYE KUBATILISHA SWALA.....37
MAMBO YA WAJIBU KWENYE SWALA.....37
NGUZO ZA SWALA.....38
KUSAHAU KWENYE SWALA.....39
SUNNAH ZINAZO AMBATANA NA SWALA ZA FARADHI.
(RAWATIBU).....40
SWALA YA WITRI.....42
RAKAA MBILI ZA ALFAJIRI.....44
SWALA YA DHUHA.....45